**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HUTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ,ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA BAJETI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA 2022/2023**

---

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu, kwa kutujaalia uzima na afya njema na hatimae tukaweza kukutana tena katika Baraza letu hili kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha nakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili tukufu, namuomba Mwenyezimungu awazidishia hekima na busara za kuendelea kuliongoza kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi aliyepo na mtangulizi wake, Katibu Mkuu ndugu Amour Harilal Bakari pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano wanayoendelea kutupatia wakati wote wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii pamoja na kazi nyengine za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao kwa kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa

nyepesi zaidi, kwa hakika wajumbe wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla | Mwenyekiti |
| 2. Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mheshimiwa Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 5. Mheshimiwa Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 6. Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 7. Ndugu Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 8. Ndugu Himid Haji Choko | Katibu |

## UKUSANYAJI WA MAPATO.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaipongeza Wizara kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato, kwani kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 wizara hii ilikadiriwa kukusanya Shilingi **4,335,056,750** ambapo hadi kufikia Machi 2022 Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi 4,775,579,496 asilimia 110% ya mapato waliyokadiriwa kutokana na vianzo vyake mbali mbali vya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Bararani pamoja na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA. Ni imani ya Kamati kwamba katika kipindi cha robo mwaka kilichabakia wizara inaweza kupiga hatua kubwa

zaidi ya makusanyo. Tunaipongeza sana Wizara kwa hatua hii.

## PROGRAMU YA USAFIRISHAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kurasimisha biashara ya usafiri wa abiria kwa njia ya pikipiki na bajaji yaani Bodaboda. Tunaiomba Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kuwafuatilia watoaji wa huduma ya usafiri huu na kukakikisha wanafanya shughuli zao kwa nidhamu na uadilifu na kuacha tabia ya kuchukua abiria kwa njia ya hatari kwani kwa kipindi kifupi tumeshuhudia ajali na vifo vingi vinanyosababishwa na usafiri wa bodaboda.

**Mheshimiwa Spika,**

Moja kati ya jukumu la Wakala wa Barabara Zanzibar ni kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote. Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inashangazwa na utekelezaji wa majukumu haya hasa katika barabara mbali mbali zilizokwisha kujengwa ambazo zimekua na mashimo ambayo yanaleta kero hasa kwa watumiaji wa vyombo vya moto. Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Barabara kuzifanyia matengenezo barabara zote ambazo zina mashimo kwa kuyaziba ili yasiendelee kuathiri watuamiaji lakini pia kuweka alama za barabara ambazo ni muhimu sana kuwepo kwa lengo la kusaidia utumiaji mzuri wa barabara na kwa usalama kwa watumiaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile tunashuhudia barabara kadhaa zikiwa zimekosa maegesho ya vyombo vya moto na kupekelekea madereva wa vyombo hivyo kuegesha magari yao kwa wanavyojisikia huku barabara hizo zikiwa na michanganyiko ya watumiaji wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu.

Aidha kumekujitokeza tatizo kwa Mamlaka inayohusika na usafi wa barabara hizo kwani hivi sasa zimekuwa zikifanyiwa usafi wakati watumiaji wa barabara wanaendelea na shughuli zao za kawaida huku wakiweka vifaa vyao vya kazi ndani ya barabara, hivyo kusababisha msongomano kwa watumiaji wa barabara hizo na pia ni hatari kwa wafagiaji wenyewe na watumiaji wa barabara kwa ujumla. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili Kamati inashauri Wizara kukaa pamoja na wahusika wa usafi wa barabara kwa kuangalia muda mzuri zaidi wa kufanya usafi huo ili kulinda usalama wao pamoja na usalama wa watumiaji wengine wa barabara hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande mwengine, hali ya usafi wa barabara zetu pamoja na jitihada hizo bado haiko vizuri kwani tunashududia michanga ikiwa imetuwama pembezoni mwa barabara pamoja na majani yakiwa yanaendelea kunawiri kati kati ya Barabara zetu. Hali hii tunadhani haileti taswira nzuri machoni mwetu pamoja na wageni.

Tunawaomba viongozi walipewa dhamana ya kuwasimamia watendaji wa usafi katika barabara zetu kuwasimamia vizuri huku watendaji nao watimize wajibu wao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali za kuikuza Sekta ya Usafiri wa Anga hasa kwa kuimarisha Viwanja vya Ndege vya Pemba na Nungwi(Kigunda) pamoja na Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume Kisauni. Hata hivyo, Kamati inasikitika kuripoti kwamba hivi sasa kumekuwa na azma ya kuifanyia marekebisho Terminal Three kwani muda mfupi tu baada ya kuanza kutumika imebainika kwamba eneo la wanaowasili (*Arrival)* ni dogo na halikidhi mahitaji ya wakati wa sasa. Hivyo, inalazimika kurejeshwa nyumba vizimba vinavyotumika na Maafisa wa Idara ya Uhamiaji pamoja na ukanda wa mizigo ili kuweza kuhami tatizo liliopo hivi sasa. Kamati inaishauri Wizara kuwa makini wakati inapoingia katika mikataba ya ujenzi wa miradi mikubwa kama hii ili kuepusha hasara

inayoweza kujitokeza kwa kipindi kifupi wakati wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunaendelea kuihimiza Serikali kukamilisha mipango ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani kwani Kamati inaamini ya kwamba kukamilika kwa mradi huo ndio suluhisho la changamoto kadhaa za kibandari zinazoikumba Zanzibar hivi sasa. Aidha tunahimiza kukamilishwa kwa bandari ya Shumba Mjini ili kuifungua Wilaya ya Micheweni kuichumi, ajira na kimaendeleo.

Vile vile tunalishauri Shirika la Bandari liimarishe huduma zake na kuhakikisha linakuwa na vifaa vyake hasa vya kupakulia mizigo na makontena kwani shughuli za kibandari zinaendelea kukuwa kila uchao ilihali vitendea kazi na mundombinu ya kibandari imebakia ni ile ile iliyopitwa na wakati na visivyokidhi haja kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea azma ya Shirika la Meli kuziuza meli zake za MV Maendeleo na MT Ukombozi II pamoja na kuikodisha meli yake ya MV. Mapinduzi II. Hatua hiyo inalenga kukabili uendeshaji wa meli hizo ambao kwa sasa unakwenda kwa hasara. Kamati inahimiza mchakato huu uharakishwe na Shirika lijipange tena ili kutafuta meli nyengine watakazoweza kumudu kusiendesha bila ya hasara.

PROGRAMU YA TECHNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

**Mheshimiwa Spika,**

Katika mwaka ujao wa Fedha, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA unakusudia kubadili mfumo wa kiuendeshaji kutoka Wakala na Kuwa Shirika. Kamati inaunga mkono hatua hii ya kimageuzi ambayo tunadhani ni nzuri katika kutoa fursa ya kukuza huduma za Mawasilino. Aidha Kamati inaunga mkono Wakala huu kuibua kianzio kipya cha mapato kwa kuanza kukusanya mapato yanayotokana na minara ya mawasiliano. Tunaziomba

taasisi nyengine kuwa wabunifu na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kukuza mfuko mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya kipekee tunaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuendelea kuwatunza wafanyakazi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kutokana na kufanyakazi katika mazingira magumu na nyeti kabisa. Mheshimiwa Spika, bila shaka Mheshimiwa Waziri anafahamu taarifa zinazohifadhiwa katika kituo kikuu cha Serikali cha kuhifadhi taarifa zake. Kadhalika, tunaiomba Serikali kuwekeza zaidi kitaaluma katika Sekta hii ya TEHAMA ili kuwaweka tayari wataalamu wachache waliopo na kukabiliana na wadukuzi pamoja na wahujumu wa mifumo ya TEHAMA kwani Technolojia ya TEHAMA inazidi kukua kila siku.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu imefarajika na Mipango ya Wizara kupitia Idara yake ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kukamilisha Upembuzi yakinifu wa Daraja la Uzi Ng'ambwa, na tunaiomba Wizara kuharakisha mapitio ya mchoro huo ili ujenzi huo uanze kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia hotuba yangu, Kamati yetu inahimiza kuendelea kwa mashirikiano baina ya Wizara na Taasisi za Muungano ziliopo Zanzibar katika utoaji wa huduma katika sekta ya mawasiliano. Kamati inazidi kutoa wito kwa Wizara kushirikiana na taasisi hizo kuendelea kutolewa elimu na kujenga uelewa kwa Wananchi wa Zanzibar ili waweze kuzitumia ipasavyo fursa zinazotolewa na taasisi hizo.

Aidha kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba yangu kwa niaba ya Kamati na

pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuipitisha Bajeti ya Wizara hii kwani imebeba sekta muhimu sana za nchi yetu ambazo ndio mategemeo makubwa ya kuinua uchumi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

**……………………**

**(Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla MAMBA ),**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano,Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**